**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

***Unapojibu tafadhali taja:***

***Kumb.Na.HW/KOG/A.20/29.VOLIV/56*** ***04 Februari, 2026***

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi tano (5) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao;

## 1.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 05

### 1.2.1 MAJUKUMU NA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwa safari za kazi;
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;
iv. Kutunza na kujaza daftari la safari “log book” kwa safari zote;
v. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;
vi. Kufanya usafi wa gari; na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 1.2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali,pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyompatia sifa ya kupata madaraja husika.Vilevile, awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na vyuo vinavyotambuliwa na serikali.

### 1.2.3 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS B**

**MASHARTI YA JUMLA**:

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45.

i) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza **Curriculum Vitae** ( CV) yenye Anwani inayotumika, namba ya simu na **Anuani ya barua pepe** (E-mail address) pamoja na majina ya Wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.

.

ii) Matokeo ya muda (Provisional/Testimonials/Statement of results) havitakubaliwa.

iii) Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

iv) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

v) Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na Wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140** wa **tarehe 30 Novemba 2010**.

vi) Waombaji wa kazi ya Dereva Daraja II wenye Leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya mafunzo vya udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.

vii) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbali mbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

viii) Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**NECTA na NACTE**).

ix) Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, wahausika watachukuliwa hatua za kisheria

x) Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.

xi) **Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 18 Februari, 2026**

xii) ***MUHIMU:*** kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),<br>
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA,<br>
S.L.P 57,<br>
**KONGWA.**

xiii) Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https:portal.ajira.go.tz/ (anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal'). Aidha, **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

**Limetolewa na**:

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, S. L. P 57, KONGWA, Simu 026-2370031, Nukushi 026-2370031, Barua Pepe: ded@kongwadc.go.tz,
Tovuti: www.kongwadc.go.tz